



UJUMBE MUHIMU KWA WAKIMBIKI NA WATAFUTA HIFADHI WOTE WANAOISHI MJINI KUHUSU VIRUSI VYA CORONA (COVID-19) (Iliyotolewa: 22 Aprili 2020)

Mnamo tarehe 15 Machi 2020 serikali ya Kenya ilitangaza hatua maalum za kuzuia kueneza zaidi virusi vya corona (COVID-19). Kutoka tarehe 27 Machi 2020, **kuna amri ya kutotoka majumbani kati ya saa moja jioni mpaka saa kumi na moja asubuhi.** Hairuhuswi kutoka nyumbani mwako wakati huu, au utakamatwa na polisi; **ama, unaweza kuwekwa na serikali katika kituo kilichoteuliwa kwa siku 14 kwa gharama yako.**

Zaidi ya hayo, mnamo tarehe 6 Aprili 2020, serikali ya Kenya ilitangaza kuwa **hakutakuwa na harakati yoyote ndani au nje ya eneo la jiji la Nairobi kutoka tarehe 6 Aprili 2020 na kaunti za Kilifi, Kwale na Mombasa kutoka tarehe 8 Aprili 2020.** Usijaribu kuingia ndani au nje ya maeneo haya au utakamatwa na polisi. Unaweza kuendelea na harakati zako ndani ya eneo unaloishi.

Unafaa kuvali maski ya uso ukiwa hadharani. Hii ni kwa usalama wako na kwa faida yako mwenyewe. Kwa kuongezea, pia utasaidia katika kupunguza kuenea kwa COVID-19. Lakini muhimu kuzingatia: Usipo vaa maski ya uso, unaweza kutozwa faini ya KES 20,000 na unaweza kukabiliwa na kifungo cha hadi miezi sita au zote mbili.

Ikiwa serikali itafanya **uchunguzi kwa wingi** katika maeneo tofauti kudhibiti kuenea kwa COVID 19 na uko mahali hapo, tafadhali **shirikiana na wafanyakazi kutoka Wizara ya Afya.**

Tafadhali usizunguke sana wakati wa mchana kama sio lazima. Ikiwa ni lazima kuzunguka, unafaa kubeba **vitambulisho vyako vya usajili** kila wakati. Zaidi, **hakikisha unafwatilia** maagizo yanayotolewa na serikali ya Kenya na hakikisha unayaafuata.

Nambari za dharura za usaidizi

- **Kwa usajili/dharura za vitambulisho:**
Sekretarieti ya masuala ya wakimbizi Shauri Moyo: 0772057770
- **Nambari ya msaada ya UNHCR:** 0800720063 (bila malipo)
- **Kwa dharura za kiafya:**
NCCK 0704873342 / 0723281352/ 0723281362
- **Kwa dharura za kisheria (kukamatwa, shida na polisi):**
Kituo cha Sheria 0720806531
- **Kwa dharura za riziki:**
Danish Refugee Council 0800720181
- **Kwa masuala yanayohusiana na NHIF (Mfuko wa kitaifa wa bima ya hospitali):**
0740049502
- **Nambari ya ushauri**
1190
- **Nambari ya GBV**
1195/ 0800720501
- **Nambari ya ulinzi wa mtoto**
116

Ukiwa na dalili zozote za COVID-19 kama homa, kikohozi, upungufu wa pumzi na shida ya kupumua, **tafadhalii wasiliana na Wizara ya Afya** kuititia 0800721316 (bila malipo); 0732353535; or 0748592558 kwa mwongozo.